BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 19 Juni, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2023/2024.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

175. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Imezoeleka kuziona gari za Serikali zikiwa na utaratibu tofauti wa usajili na gari za watu binafsi. Hata hivyo, utaratibu huo haufahamiki sana na wananchi walio wengi.

Je, ni utaratibu upi unaotumika kuzisajili gari za viongozi wa Serikali.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

192. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwenye kisiwa cha Tumbatu iko gati ndogo ambayo inawasaidia wana Tumbatu na wageni wengine wanaokwenda huko kushukia na kupandia vyombo mbali mbali. Hata hivyo, hali ya gati hiyo si ya kuridhisha.

(a) Kwa kuwa gati hii imo katika mazingira mabaya sana na hatarishi kwa wanachi hao. Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya walau kuifanyia matengenezo madogo gati hiyo, ili kuweza kuepusha madhara kwa wananchi wetu hawa.

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba hali ya gati hiyo ni mbaya sana kiasi kwamba kuikanyaga sio salama na haikanyagiki bila kuvaa viatu.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuiboresha kwa kuitengeneza gati hiyo, ili iwe salama kwa matumizi ya binaadamu wa kawaida.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi:**

202. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Pamoja na jitihada za Serikali za kuongeza makaazi ya wananchi katika visiwa vya Unguja na Pemba, bado kuna upungufu wa makaazi ya wananchi kinyume na ilivyodhamiriwa wakati wa Mapinduzi.

(a) Je, ni ipi takwimu ya mahitaji ya nyumba za kuishi kwa Unguja na Pemba hadi sasa.

(b) Je, ni upi mpango wa Serikali katika kukamilisha nyumba za kuishi kulingana na mahitaji ya Zanzibar.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuweka mazingira yatakayowezesha kampuni binafsi kujenga majengo ambayo wananchi watakuwa wanalipa kidogo kidogo au kwa mkupuo ili kupata umiliki wa nyumba za bei rahisi na zenye ubora.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

171. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Mashindano ya uandishi wa vitabu vya riwaya na tamthilia yanayofanyika nchini, yamekuwa chachu ya kukijengea heshima Kiswahili ndani na nje ya nchi.

(a) Ni lini Serikali yetu ya Zanzibar kupitia Wizara husika itafikiria kuanzisha mashindano kama haya.

(b) Ni waandishi wepi wa Kiswahili wamewahi kuchukua tunzo kwa ushiriki wao kwenye mashindano kama haya, ndani na nje ya nchi.

(c) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwaenzi waandishi hao kwa lengo la kuuendeleza ujuzi kwa waandishi wachanga.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

136. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Sekta ya Kilimo ni muhimu sana kwa kuukuza uchumi wetu, ambayo pamoja na mambo mengine muhimu, suala la wakulima kuwa na taarifa mbali mbali za maendeleo ya kilimo na umuhimu wake, ni jambo linaloangaliwa kwa upekee wake.

Je, Wizara yako inatumia vipi teknolojia ya TEHAMA katika kuwapatia wakulima taarifa mbali mbali zenye tija katika sekta ya kilimo.

227. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ili kuweza kuleta tija kwa wafugaji, wananchi na Serikali kwa ujumla, ni vyema kuimarishwa kwa afya ya mifugo kwa kutumia njia na tiba za kisasa. Hata hivyo, jambo hilo linahitaji kupewa uzito zaidi na Serikali kuliko ilivyo sasa.

(a) Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuboresha huduma za matibabu ya wanyama, upatikanaji wa madawa, chanjo, mbegu pamoja na kujenga majosho na machinjio mapya bora na ya kisasa.

(b) Je, Serikali inatumia njia gani kuongeza nafasi za masomo ya udaktari wa mifugo pamoja na kuwavutia madaktari waliopo sasa na madaktari watarajiwa wa wanyama.

(c) Je, Serikali imetoa maeneo mangapi ya kuanzisha ufugaji (ranches) kwa wawekezaji wa ndani na nje ili waweze kufuga kibiashara.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

173. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na ongezeko la watu wenye matatizo ya ugonjwa wa akili nchini, kiasi ambacho mara nyengine unaweza kushuhudia wagonjwa kadhaa wakitembea barabarani na sehemu nyengine mbali mbali.

(a) Je, tathmini ya ongezeko la watu wenye matatizo ya ugonjwa wa akili ikoje kwa sasa.

(b) Je ni kweli kwamba kina baba ndio wenye ongezeko kubwa kuliko kina mama na ni kwa nini.

(c) Upi mpango mkakati wa Wizara wa kuondokana na tatizo hilo.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

230. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali imekuwa ikikwama katika kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo kwa sababu mipango ya utambuzi, usajili, ufikiwaji na uwezeshaji wawashiriki wa uvuvi haikuwa imara wala haikuwa rasmi.

(a) Je, ni lini kwa mara ya mwisho Serikali ilifanya sensa rasmi na ya uhakika ya madiko na masoko ya wavuvi kwa ajili ya mipango ya utambuzi, usajili, ufikiwaji na uwezeshaji wa

washiriki wa uvuvi.

(b) Je, ni yepi matokeo ya sensa ya karibuni ya Serikali kuhusiana na madiko na masoko ya wavuvi.

(c) Je, kwa kiwango gani cha kibiashara Serikali imewawezesha wafanyabiashara wadogo wadogo katika ufugaji wa samaki na viumbe vya baharini kama vile kamba, kaa, na majongoo.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

168. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Nchi nyingi duniani zinatambulika kutokana na alama mbali mbali zinazobeba historia pana za nchi zao (icons). Kwa mfano nchi ya Ufaransa hutambulika kutokana na mnara wa Paris (The Eiffel Tower) na nchi ya China inatambulika kutokana na ukuta wake mkuu (The Great Wall).

(a) Je, ni upi utambulisho wa alama za kihistoria zinazoitambulisha Zanzibar duniani.

(b) Ni upi umuhimu wa alama hizo kwa ustawi wa uchumi na historia ya nchi yetu.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**19 Juni, 2023.**

**(Abdalla Ali Shauri)**
**Kny. KATIBU WA BARAZA**